JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI
MASASI GIRLS' SECONDARY SCHOOL

Head office
P.O.Box 53,
Masasi

"**TENDA BILA KUSUKUMWA**"
IS OUR MOTTO

Email;masasigirls70@gmail.com

Makamu Mkuu wa Shule : 0688399725
Matron : 0712646372
Taaluma 0787754925

Tarehe 19/05/2021

Jina la Mwanafunzi……..…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MASASI HALMASHAURI YA MJI MASASI MKOA MTWARA MWAKA 2021/2022

1.0. Kwa niaba ya kamati ya uchaguzi ninayo furaha kukuarifu rasmi kwamba umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha **tano** Tahasusi ya…….. mwaka**2021/2022**.**TENDA BILAKUSUKUMWA**" maneno hayo ndiyo **KAULI (MOTTO**) au mwongozo wa shule yetu. Ukiwa umekubali kujiunga na shule hii basi huna budi kuitafakari kauli hiyo.
Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi ipo umbali wa kilometa moja na nusu Magharibi mwa mji wa Masasi. Usafiri kutoka mjini Masasi kuja shuleni unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi/stend kuu. Nauli ni shs. 1,000/= kwa pikipiki na 2,000 kwa Bajaji.Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **5/7/2021**Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe**4/5/2021**na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/7/2021**

Muhimu:Endapo utachelewa zaidi ya wiki mbili utakuwa umepoteza nafasi hii.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare ya shule

(a) Sare za darasani ni:
- Sketi Mbili Rangi ya bluu nyeusi(darkblue)-Rinda Box, Isteem namba moja ni nzuri zaidi.Picha ya mshono imeambatanishwa, ni lazima sketi iwe ndefu kama inavyoonekana kwenye picha ya mshono.
- Shati nyeupe mikono mifupi na isiyobana **[WAKRISTO].** Nusu kanzu na hijab[**Kijub**] nyeupe isiyofunika goti, mikono mirefu **[WAISLAM]** jozi mbili
- Raba nyeupe za kufunga na kamba zenye kisigino kifupi jozi mbili
- Soksi nyeupe zisizo na urembo au alama zozote za rangi angalau jozi mbili.
- Sweta rangi ya **dark blue**mikono mirefu isiyo ya kola

(b) Sare za kushindia**[Shamba dress]** ni gauni yenye mikono mifupi rangi ya **light blue**mbili.Picha ya mshonoIsteem namba mojani nzuri zaidi[**imeambatanishwa**]. Ni vema hijabu kwa Waislam iwe nyepesi na ifanane na sare ya kushindia[**shamba dress**]

(c) Sare za michezo ni T-shirt rangi ya grey **[Kijivu]**yenye kola [mbili]. **(Hizi zinapatikana shuleni kwa shilingi 12,000/= zikiwa na nembo ya shule)** na Truck suit nyeusi isiyobana mwili yenye mchirizi mweupe pembeni na raba nyeusi.

(d) Tai ndefu mbili isivuke kitovu **[rangi ya dark blue]**ifanane na rangi ya sketi ya shule**[kwa Wakristo]**

Muhimu:
Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni. Aidha mwanafunzi anaposafiri kuja shuleni avae sare ya shule.

2.2 **Ada na michango ya shule**:

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000/=** au Shs. **35,000/=**kwa nusu mwaka

(b)Michango inayotakiwa kulipwa na kila mwanafunzi

i.Kitambulisho na picha…….Tshs 6,000/=
ii. Tahadhari …….Tshs 5,000/=**[Haitarejeshwa]**
iii.Mchango wa ukarabati wa samani ……...Tshs 15,000/=
iv.Taaluma kwa mwaka …….Tshs 20,000/=
v.Mchango wa walinzi,wapishi na vibarua kwa mwaka …..Tshs 30,000/=
vi.Nembo ya shule sh ……. Tshs 2,000/=
vii.Mchango wa huduma ya afya shuleni ……...Tshs 10,000/= (huduma ya kwanza Tshs 5000/=,(kwa wenye bima ya AFYA watalipia Tshs 5,000/= tu ya huduma)
viii.Mtihani wa pamoja wa Mkoa kidato cha Tano ……..Tshs 20,000/=
ix. Mahafali …….Tshs 10,000/=(kwa mwaka)
x. Mchango wa Umisseta ……..Tshs 5,000/=(kwa mwaka)

MUHIMU:

- Ulipaji wa ada na michango yote ufanyike kwa njia ya Benki (**NMB**)

Jina la akaunti ni**MASASI GIRLS SECONDARYSCHOOL.**
Ada ilipwe **ACCOUNT NO. 70501200104**.

- **Michango mingine** ilipwe kwenye **ACCOUNT No.70501200174.**

- **KWA KUWA SHULE INATUMIA MIFUMO YA FEDHA YA SERIKALI,TUNAOMBA ADA NA MICHANGO YOTE ILIPWE KUANZIATAREHE 01/07/2021 YAANI MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

- Tafadhali wasiliana na karani wa Benki aandike kuwa ni **Ada** au **Michangomingine**. Usisahau kuandika jina kamili laMwanafunzi .Risiti (paying slip) iletwe kwa Mhasibu siku ya kufungua shule, **(mara tu mwanafunzi anaporipoti shuleni).**

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni

i.Madaftari 10 caunter book ,kalam na mkebe wa hesabu
ii.Shuka mbili rangi nyeupe,blanket 1,foronya 1,chandarua 1
iii. Nguo za ndani za kutosha (chupi, shimizi, sidiria, Tight fupi rangi nyeusi au nyeupe)
iv.Ream ya karatasi 1 (SizeA4) kwa mwaka
v. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika(Orodha imeambatanishwa)
vi.Dissecting kit kwa mwanafunzi wa Biolojia
vii.Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi na Jiografia .
viii) Laboratory Coat(Nyeupe) linalovuka magoti kwa wanafunzi wa sayansi.
ix).Godoro la futi $2\frac{1}{2}$ ftx 4
x). Mafuta ya kupaka yasiyo na viambata vya sumu**[cream]** na harufu kali.
xi)Kanga au kitenge (jozi moja tu)
xii)Chandarua rangi nyeupe, Taulo, Mswaki , Dawa ya meno, Sabuni yakufulia na kuogea.
xiv) Nakala ya hati ya Matokeo kidato cha iv au" Result slip".
xv). Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
xvi). Picha ya mwanafunzi 1, ya wazazi /walezi mojamoja, na ndugu wa karibu wamwanafunzi picha moja
xvii).Vyombo vya chakula[Sahani,Bakuli,Kijiko na Kikombe]
xviii).Ndoo mbili ndogo zenye mfunikona kikopo cha kuogea

VIFAA VYA USAFI AMBAVYO MWANAFUNZI ANATAKIWA AJE NAVYO:

(a) Wanafunzi wote wanatakiwa waje na Sabuni ya maji kwa ajili ya kusafishia choo (Lt 5) , Fagio Laini(Soft broom) na Fagio ya wima ya kufagilia nje(Chelewa).

(b) Vifaa vifuatavyo viletwe kulingana na TAHASUSI kama ilivyo katika jedwali,

TAHASUSI	VIFAA
HGK	Jembe lenye mpini na Kwanja (Fyekeo)
HGL	Fagio ngumu(Hard broom) na brush fupi ya chooni
HKL	Kwanja(Fyekeo) na Chepe (Sepetu)
CBG	Mopa (za kukaushia maji) na Reki
PGM	Panga na Jembe lenye mpini
PCB	Jembe lenye mpini na Kwanja (Fyekeo)

5.0 Sheria za shule

a.Wanafunzi wanapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote

b.Kuheshimu ukumbi wa Mkutano, Mahali pa chakula, Ofisi za shule na Jiko la shule n.k.

c. Kuweka shule na maeneo yake yote katika hali ya Usafi wakati wote

d. Kuwahi katika mikusanyiko na kila mahali wanapotakiwa

e.Wanafunzi wanapaswa kuwa wakimya Madarasani, wakati wakijisomea na Mabwenini.

f.Wanafunzi wanapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na Mkuu wa shule au Msaidizi wake

g.Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya Mkononi , Redio na Pasi ya Umeme shuleni.

h.Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu popote bila kibali cha uongozi wa shule ili kuepuka upelekaji wa taarifa zisizo sahihi kwa wazazi.

i.Wanafunzi hawaruhusiwi kuja, au kuletewa chakula cha aina yoyete toka nyumbani.

j.Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mazungumzo na ndugu yake msikitini,kanisani au hospitalini. Kama ndugu huyo ana maagizo afike ofisini aonanena uongozi wa shule.

k.Wanafunzi hawaruhusiwi kwenda nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalum.

l.Mafuta yenye harufu kali, rangi za kucha, wanja, curl nywele na mapambo kama bangili n.k. haviruhusiwi kwa mwanafunzi.

m.Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa na wimbo wa taifa.

n.Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au kazi (wagonjwa watakaa chumba maalum).

o.Wanafunzi hawaruhusiwi kusuka nywele. Wanatakiwa kuwa nanywele fupi wakati wote wawapo shuleni na si K IDUKU au kipara

p.Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo hapa shuleni.

q. Yawapasa wanafunzi wote kushiriki michezo/ mazoezi ili kulinda afya Zao

r. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoboa masikio wawapo shuleni.

MUHIMU ;

- Wanafunzi wote ni lazima kuanza safari mapema na kuripoti Shuleni siku ya kufungua Shule Wakiwa na tiketi zao zinazoonyesha jina,tarehe halali ya kusafiri, Na mwisho wa mapokezi hasa wakati wa kutoka likizo ndogo/kubwa ni saa10;00 jioni,
- Ni wajibu wa mzazi kutoa taarifa ya mwanaye kuchelewa kuripoti siku husika kwa uongozi wa shule kabla ya shule kufunguliwa ili kuondoa usumbufu kwa shule na mwanafunzi na hata mzazi.
- Na endapo mawasiliano kati ya Shule na Mzazi hayatafanyika kwa wakati, Mzazi atalazimika kumleta mwanaye shuleni na kutoa maelezo la sivyo hatopokelewa

6.0: MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi

ii. Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi

iii. Kuharibu makusudi mali ya umma na watu wengine

iv. Kuolewa.

v. Utoro wa siku 90 bila taarifa

vi. Biashara, ulevi na kutumia dawa za kulevya
vii. Kuwa na mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
viii. Kuingia na kushiriki kwenye vilabu vya pombe, nyumba za kulala wageni.
ix. Kugoma na kuhamasisha mgomo
x. Kunyoa nywele katika mtindo usiokubalika .Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
xi.kutao lugha chafu kwa Wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
xii. Kudharau bendera ya Taifa.
xiii.Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria ya Nchi.
xiv. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xv.Uasherati, Ubakaji, Ushoga, Kusagana na Ulawiti.
xvi. Kukaa/kulala bwenini wakati wa vipindi (Preparation) au wakati wa kazi za nje
xvii.Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu,kujinyonga n.k

Fomu hii ya kujiunga na shule inatakiwa irudishwe ofisini pamoja na cheti cha kupima kilichojazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali ambacho pia kimeambatanishwa. Hakikisha umetoa nakala ya fomu hii kwa ajili ya rejea yako.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....

MPEMWANA M.
MKUU WASHULE

MKUU WA SHULE

Masasi Girls High School,
P.O. Box 53,
MASASI
Ref. No. …….. **Date ……..**

PART A:
To the Medical Officer,
…….
…….
…….

REF: …….
Please examine the above named student as to her physical and mental fitness for being student. Each defect will hinder a girl for Secondary School Education.

1. (a) Eye sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (d) Speech
   (e) Venereal Disease
   (f) Leprosy
   (g) Epilepsy
2. Neurosis
3. Other serious diseases
4. Pregnancy

PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a GOVERNMENT MEDICAL OFFICER):
I have examined the above named student and consider that she is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.

(a) Eye sight …… (f) Leprosy …….....
(b) Hearing ……. (g) Epilepsy …….
(c) Limbs……. (h) Neurosis …….
(d) Speech …… (i) Other serious disease ……..
(e) Venereal diseases ……. (j) Pregnancy ……

Date…….. **Signature……**

Station …… **Designation …….**

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina la Kamili……
(kama lilivyo kwenye self form)
2. Tarehe ya kuzaliwa…….....
3. Anwani ya nyumbani……
4. Mahali unapoishi(nyumbani kwenu) : Wilaya…….....Tarafa…….
   Kata…….Kijiji…….
5. Shule ya sekodari uliyotoka……
6. Dini……...
7. Kabila……...
8. Taifa(Mtanzania/Si Mtanzania)……...

PICHA

9. Jamaa katika familia(Watakaohusishwa katika malezi ya mwanafunzi akiwa hapa shuleni)

(i) Jina la Baba……...
Anuani……Namba ya simu……..
Anaishi/Haishi……...
Kazi yake……...

PICHA

(ii) Jina la Mama…….
Anuani……Namba ya simu……..
Anaishi/Haishi……...
Kazi yake……...

PICHA

(iii) Jina la Mlezi/Ndugu…….
Anuani……Namba ya simu……..
Anaishi/Haishi……...
Kazi yake……...

PICHA

10. Mkataba wa Mwanafunzi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

Mimi……. (Mwanafunzi) nakiri kuwa, nimezisoma sheria, kanuni na taratibu za shule kwa umakini na utulivu mkubwa. Hivyo basi ninaahidi: “Nitazifuata Sheria, Kanuni na Taratibu za shule kama zilivyoelekezwa Aidha ninaamini kuwa Sheria na Taratibu zipo kwa nia ya kunisaidia katika Nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu, maadili na taaluma.” Vilevile naahidi kuwa sitoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

…….. ……...……
Sahihi ya mwanafunzi Tarehe

11. Form ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yaliyotolewa na shule

Mimi……(Mzazi/Mlezi) wa Mwanafunzi…….. Ninakiri kuwa, nakubaliana na sheria, kanumi na maelekezo yote yaliyotolewa na shule. Hivyo basi niko tayari mtoto wangu asome katika shule hii nitakuwa tayari kumpa kila aina ya msaada utakaohitajika katika kufanikisha masomo yake na malezi yake kwa ujumla akiwa hapa shuleni kwa kipindi cha miaka miwili (2).

…….. ……...……
Sahihi ya Mzazi/Mlezi Tarehe

ORODHA YA VITABU (NUNUA KULINGANA NA MASOMO YAKO)

1. MATHEMATICS (ADVANCED MATHEMATICS AND BAM)

- **ADVANCED MATHEMATICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS FV (Septine I. Sillem) - gdy publication.**
- **ADVANCED MATHEMATICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS FVI (Septine I. Sillem) - gdy publication.**
- **PURE MATHEMATICS 1&2 , J.K BACKHOUSE.**
- **BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS FV (Septine I. Sillem) - gdy publication.**
- **BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS FVI (Septine I. Sillem) - gdy publication.**

2. PHYSICS.

- **PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS XI S. CHAND.**
- **ADVANCED PHYSICS, Rogers Muncaster.**

3. CHEMISTRY.

- **A TEXT BOOK FOR CBSE CHEMISTRY FOR CLASS XI AND XII, S. CHAND.**
- **CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASSXI AND XII, S. CHAND.**

4. BIOLOGY.

- **BIOLOGICAL SCIENCE 3rdEDITION, D.J TAYLOR, N.P.O GREEN.**
- **BIOLOGY FOR CLASS XI , S. CHAND**

5. ENGLISH LANGUAGE

- **ADVANCED LEVEL ENGLISH; A PRACTICAL APPROACH –NEW EDITION, NICHOLOUS ASHELI.**
- **ANALYSIS OF LITERARY WORKS, NYAMBARI NYANGWINE.**

6. HISTORY

- **HISTORY PAPER ONE FOR ADVANCED LEVEL, SALEHE YASIN.**
- **ESSENTIALS IN ADVANCED LEVEL HISTORY PAPER 2, SALEHE YASIN.**

7. KISWAHILI

- **NADHARIA YA LUGHA YA KISWAHILI KIDATO CHA 5 NA 6, SALAHAYA M.C (2016)**
- **NADHARIA YA FASIHI KIDATO CHA 5 NA 6, NYAMBAARI NYANGWINE.**
- **TAHAKIKI KIDATO CHA TANO NA SITA, NYAMBARI NYANGWINE.**

8. GEOGRAPHY:

- **KAMILI .Z. (2016) PRACTICAL GEOGRAPHY ALIVE**
- **MSABILA D.T. (2018) A COMPREHENSIVE APPROACH TO PHYSICAL GEOGRAPHY FOR SECONDARY SCHOOL, DAR ES SALAAM, TANZANIA**
- **MTEGETWA M. (2001) GEOGRAPHY MAP SHEET PREPARATION FOR ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**
- **MSABILA D.T. (2018) AN INTERGRATED REGIONAL STUDY ON HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY ADVANCED LEVEL PAPER 2**

9. GENERAL STUDIES

- **BIGIRWAMUNGU J. (2010) UNDERSTANDING GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL, AFRICA PROPER NETWORK, DAR ES SALAAM TANZANIA**

- **NYANGWINE C.M. (2018) ADVANCED LEVEL GENERAL STUDIES NOTES FORM 5 & 6 DAR ES SALAAM TANZANIA**

- **KAMILI Z. (2017) GENERAL STUDIES ALIVE KAMILI BOOKS AND GENERAL SUPPLIES DAR ES SALAAM TANZANIA**

- SARE ZA SHULE



-SARE ZA SHULE



SARE YA KAZI



SARE YA KARI